**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2025/2026

**ILIYOWASILISHWA NA**


**MHE. SHAABAN ALI OTHMAN (MBM)**

**WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**


**JUNI, 2025**

# VIONGOZI WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

# ZANZIBAR



**Mhe. Shaaban Ali Othman**
**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi**
**Zanzibar**



**Captain, Hamad Bakari Hamad**
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi**
**Zanzibar**



**Nd. Zahor Kassim Mohammed El-kharousy**
**Naibu Katibu Mkuu**
**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi**
**Zanzibar**

# YALIYOMO

HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ............. 1
UTANGULIZI ............................................................ 1
UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU KATIKA PATO LA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............................................. 3
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025 ............................................ 8
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025 ......................................................... 9
MAFANIKIO YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ................ 11
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............................................. 16
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ........................................................ 16
PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU. ............................................. 17
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA (ZPRA)I ................................ 20
KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPDC). ................................................ 23
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI .................. 25

PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI ................................ 27
TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR - ZAFIRI .......................................... 31
KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR – ZAFICO ......................... 35
MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU - DSFA ................................................................ 37
PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MALIASILI ZA BAHARI .................................................................. 40
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI...................... 44
PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI........ 45
PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI ...... 47
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA. 49
CHANGAMOTO...................................................................... 52
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026......................................................................... 53
MAKADIRIO YA MATUMIZI 2025/2026................................ 53
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA ...................... 55
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .................... 56
MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2025/2026............................... 58
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU .......................................................................... 60

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA MAENDELEO
YA UCHUMI WA BULUU ....................................................61
PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAFUTA
NA GESI ASILIA ...............................................................62
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI
WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA)..................64
KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA
ZANZIBAR, ZPDC...............................................................65
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI ....................67
PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA
UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI ..................................67
TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA
BAHARINI ZANZIBAR (ZAFIRI) ..........................................69
KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR - ZAFICO..........................70
MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU -DSFA ......71
PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MALIASILI ZA BAHARI.......73
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA
YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ..............................................74
PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI.................75
PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI ...............76
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA
SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA.............78
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA
WA FEDHA 2025/2026. ..........................................................79
HITIMISHO .........................................................................80
VIAMBATISHO.....................................................................86

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu, lipokee, lijadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo yanawasilishwa katika Mfumo wa Programu (PBB)

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki kinachojadili makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa anaoutoa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Shukurani za pekee zimuendee Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi, kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, mashirikiano, usalama, amani na utulivu. Hatua hiyo imepelekea utekelezaji mzuri wa malengo ya Serikali na maelekezo yake anayoyatoa katika kuleta maendeleo ya Sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hatimae kukuza Uchumi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufikia azma yake ya kuinua uchumi na maisha ya Wazanzibari. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwashauri vyema viongozi wetu na kufanya maamuzi mema yenye hekima na busara katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kwa dhati kabisa kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi. Pia, nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

6. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo, pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hio, kwa miongozo na ushauri wanayoendelea kuitoa kwa Wizara yetu katika kuhakikisha inafanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2024/2025, na kuendelea kutusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Napenda kuihakikishia Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo mliotupatia yatazingatiwa katika kukamilisha bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## UKUAJI WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

7. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaendelea na kazi ya kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kiuchumi kupitia sekta ya Uchumi wa Buluu. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi umezingatia maelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar

(ZADEP) 2021-2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu (Agenda 2030) hususan Lengo Namba 14, Mpango wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Afrika kupitia lengo nambari 6, ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025, pamoja na maelekezo na Ahadi za Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatekeleza kazi zake kupitia Sera ya Uchumi wa Buluu na Mkakati wake wa Utekelezaji, Sera ya Mafuta na Gesi Asilia, Sera ya Uvuvi na Mkakati wake wa Utekelezaji na Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia, Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar.

8. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar (2022), kwa kusimamia na kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari na kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi kuhusiana na fursa za Uchumi wa Buluu ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko pamoja na kuchangia katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, mwani, uhifadhi wa

bahari, utafiti wa uvuvi na bahari, biashara za baharini, utalii, mafuta na gesi asilia pamoja na nishati mbadala. Lengo hilo linatekelezwa katika nyanja kuu tatu zifuatazo:

- **Uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini:** Kuendeleza uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo uvuvi mdogo mdogo, wakati na bahari kuu, ukulima wa mwani na ufugaji wa majongoo bahari. Pamoja na kuvutia uwekezaji mkubwa katika sekta ya uvuvi na ukulima wa mwani kwa kujenga miundombinu ya uvuvi na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya baharini.

- **Maendeleo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia:** Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo ya baharini na nchi kavu kwa kushirikiana na wewekezaji na kuhakikisha kwamba wazawa wanafaidika na uwekezaji huo katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

- **Uratibu wa shughuli zote za Uchumi wa buluu:** Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu kwa kupitia mpango mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu. Wizara inaendelea na juhudi za kuwaunganisha wadau wote wa sekta za Uchumi wa buluu wa ndani na nje ya nchi, ikiwemo sekta ya

utalii, usafiri wa baharini na miundombinu ya bandari, Usimamizi na uhifadhi wa Mazingira, Ulinzi wa baharini na sekta nyenginezo. Pia, wizara inashirikiana na taasissi nyengine ikiwemo ZIPA katika utafutaji wa wawekezaji wakubwa katika sekta za Uchumi wa Buluu ili kutoa ajira na kukuza Uchumi wa Zanzibar.

9. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha uzalishaji wa samaki kimeongezeka kwa asilimia **107.2** kutoka Tani **38,107** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 205.35** (2020) hadi kufikia Tani **78,943** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 618.18** (2024) (**Kiambatisho Nam. 1**). Aidha, Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kwa asilimia **124.6** kutoka tani 8,785 zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 5.387** (2020) hadi kufikia tani 19,716 zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 16.14** (2024) **(Kiambatisho Nam. 2).**

10. **Mheshimiwa Spika,** Mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.1 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia **5.7** mwaka 2024 (OCGS 2024). Aidha, Sekta ya uvuvi imekua kwa asilimia **14.2** kwa mwaka 2024 kutoka asilimia **8.1** mwaka 2023. Ongezeko hili linatokana na hatua mbalimbali za Serikali katika kuimarisha sekta ya Uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi, wakulima wa mwani na

wafugaji wa mazao ya baharini kwa kuwapatia nyenzo za kisasa, masoko na kuimarisha usimamizi wa hifadhi za bahari.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imefanikiwa kuwasilisha Serikalini Waraka wa Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 na kutunga Sheria ya Maendeleo ya Uvuvi kwa lengo la kusimamia, kuendeleza na kuratibu matumizi ya rasilimali za uvuvi Zanzibar. Aidha, kukamilika kwa Sheria hii kutapelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar.

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kukamilisha utayarishaji wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wavuvi, vyombo vya uvuvi pamoja na ukataji wa leseni za uvuvi ambapo tayari mfumo huo umeanza kufanyakazi.

13. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio makubwa yameendelea kupatikana katika sekta ya uchumi wa bukuu ambapo kwa kushirikiana na Serikali Jamhuri ya watu wa Korea, Wizara tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Shumba Mjini Kisiwani Pemba na Chuini Unguja. Aidha, kazi ya ujenzi wa bandari kwa

upande wa Shumba Mjini imepangwa kuanza katika mwaka wa Fedha 2025/2026.

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar imekamilisha zoezi la majaribio la Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari (MSP) katika eneo la Zone 5 liliopo katika hifadhi ya Mkondo wa PECCA.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, mafanikio makubwa yameendelea kupatikana kwa kutangaza vitalu 10 (8 Baharini na 2 nchi kavu) kwa wawekezaji kupitia majukwaa na mikutano mbambali ya kimataifa. Aidha, Wizara imefanikiwa kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya usimamizi wa taarifa za Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo ujenzi wa kituo maalumu cha kuhifadhia na kukagulia taarifa za mafuta na Gesi Asilia pamoja na ununuzi wa vifaa vinavyohusika na uhifadhi wa taarifa hizo.

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu

ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

17. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia programu hizo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipanga kutekeleza jumla ya Miradi nane (8) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 55.027** (**Kiambatisho Nam. 3**).

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilikadiriwa kukusanya Mapato ya jumla ya **Shilingi Bilioni 5,921,734,000** kutoka vianzio vyake vitano(5) vya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 4,134,779,699** sawa na asilimia **70** ya makadirio. Ambapo Unguja ni **Shilingi Bilioni 4,046,515,749** na Pemba ni **Shilingi Milioni 88,263,920** (**Kiambatisho Nam.4**).

19. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni**

**66,012,766,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 10,985,000,000** kwa Kazi za Kawaida na **Shilingi Bilioni 55,027,766,000** kwa Kazi za Maendeleo.

20. **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyiko wa fedha kwa Kazi za Kawaida ni **Shilingi Bilioni 10,985,000,000;** Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 4,130,200,000** Mishahara, **Shilingi Bilioni 2,501,400,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 4,353,400,000** ni ruzuku kutoka SMZ ambapo **Shilingi Bilioni 1,177,700,000** ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari Zanzibar (ZAFIRI), **Shilingi Bilioni 2,788,900,000** kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na **Shilingi Milioni 386,800,000** kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO).

21. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2025, fedha zilizopatikana ni **Shilingi Bilioni 28,482,447,160** sawa na asilimia **43** ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 6,088,828,561** ni kwa kazi za kawaida, ambapo **Shilingi Milioni 700,473,036** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi Bilioni 2,695,544,182** ni Mishahara na **Shilingi Bilioni 2,692,811,344** ni Ruzuku kutoka SMZ.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara imeingiziwa jumla ya **Shilingi Bilioni 22,393,618,599.** Ambapo **Shilingi Bilioni 21,045,628,337** kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 1,347,990,262** kutoka Washirika wa Maendeleo (**Kiambatisho Nam. 5**).

## MAFANIKIO YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

23. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitekeleza programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:

   i. Kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa samaki kwa asilimia **107.2** kutoka Tani **38,107** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 205.35** mwaka 2020 hadi kufikia **Tani 78,943** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 618.18** mwaka 2024. Vile vile, Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kwa asilimia **124.6** kutoka tani **8,785** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 5.387** mwaka 2020 hadi kufikia **tani 19,716** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 16.14** mwaka 2024.

   ii. Mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.1 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia **5.7** mwaka 2024 (OCGS 2024). Aidha, Sekta ya uvuvi imekua kwa asilimia **14.2** kwa mwaka 2024 kutoka asilimia asilimia **8.1** mwaka 2023.

iii. Wizara imefanikiwa kuwasilisha Serikalini Waraka wa Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 na kutunga Sheria ya Maendeleo ya Uvuvi kwa lengo la kusimamia, kuendeleza na kuratibu matumizi ya rasilimali za uvuvi Zanzibar. Aidha, kukamilika kwa Sheria hii kutapelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari Zanzibar.

iv. Kwa kushirikiana na Serikali Jamhuri ya watu wa Korea, Wizara tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Shumba Mjini Kisiwani Pemba na Chuini Unguja. Aidha, kazi ya ujenzi wa bandari kwa upande wa Shumba Mjini imepangwa kuanza katika mwaka wa Fedha 2025/2026.

v. Katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, Kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), Serikali imetangaza jumla ya vitalu 10 vya Mafuta na gesi Asilia (8 Baharini na 2 nchi kavu) kwa wawekezaji kupitia majukwaa na mikutano mbali mbali ya kimataifa.

vi. Wizara imefanikiwa kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya usimamizi wa taarifa za Mafuta na Gesi Asilia ikiwemo ujenzi wa

kituo maalumu cha kuhifadhia na kukagulia taarifa za mafuta na Gesi Asilia pamoja na ununuzi wa vifaa vinavyohusika na uhifadhi wa taarifa hizo.

vii. Wizara pia imefanikiwa kukamilisha utayarishaji wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wavuvi, vyombo vya uvuvi pamoja na ukataji wa leseni za uvuvi ambapo tayari mfumo huo umeanza kufanyakazi.

viii. Wizara imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki katika eneo la Kama Unguja na kufunguliwa rasmi Katika Maadhimisho ya miaka 61 ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

ix. Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi imefanikiwa kuanzisha Maabara ya kisasa ya uzalishaji wa mbegu za mwani (Tissue Culture Laboratory) katika eneo la Beit El Raas pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara. Maabara hii itasaidia kupatikana kwa mbegu bora zinazostahamili mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza uzalishaji. Aidha, mradi pia, umekamilisha utafiti wa kutambua mbegu bora za mwani zinazopatikana Zanzibar kwa lengo la kuanzisha vitalu vya mbegu za mwani ili kutatua changamoto za upatikanaji wa mbegu kwa wakulima wa mwani Zanzibar.

x. Katika kuimarisha ubora wa zao la mwani na kupunguza upotevu wa zao hilo wizara kupitia Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi imekamilisha ujenzi wa chanja 140 za kuanikia mwani na kuwakabidhi wananchi. Kati ya hizo chanja 97 Muungoni kwa Unguja na 43 Kiuyu Mbuyuni Pemba. Aidha, jumla ya makaushio 2 ya kuanikia mwani (solar dries) kwa upande wa Unguja na Pemba yamekamilika.

xi. Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi imesomesha jumla ya wakulima wa mwani 3,100 juu ya mbinu bora za ukulima wa mwani katika kina kirefu kwa kutumia njia ya kamatia chini (double loop techniques) kwa upande wa Unguja na Pemba. Aidha, programu imekamilisha kuandaa mitaala ya kusomeshea (training material) kwa wakulima wa mwani. Pia, kupitia mradi wa IFAD Wizara imekamilisha ununuzi wa vifaa vya kuanzisha vitalu vya mashamba ya mwani (seaweed nursery) Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

xii. Vile vile, Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi imefanikisha kuanzisha/kuunda kamati ya mwani ambayo imejumuisha wadau mbali mbali

kutoka Serikalini na Sekta binafsi kwa lengo la kujadili masuala mazima ya ukulima wa mwani ili kuwasaidia wakulima hao kuepukana na changamoto wanazokutana nazo katika uzalishaji na usarifu wa zao hilo.

xiii. Katika kuimarisha upatikanaji wa vifaranga vya majongoo bahari Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Zanzibar Marine Hatchery ambapo wizara ina ubia wa asilimia 49, jumla ya vifaranga 1,500,000 vya majongoo bahari vimezalishwa, kati ya hivyo vifaranga 80,000 vimegawiwa kwa wafugaji Unguja na Pemba. Aidha, Hatchery inaendelea na utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuuza vifaranga vya majongoo bahari.

xiv. Katika utekelezaji wa ukondoishaji wa masuala ya Mpango Makhsusi wa Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Planning), Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar imekamilisha zoezi la majaribio la MSP katika eneo la Zone 5 katika hifadhi ya mkondo wa Pemba (PECCA).

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

24. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Programu zake kuu tatu (3) na Programu ndogo sita (6) ni kama ifuatavyo;

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

25. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii ina programu ndogo moja nayo ni Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na ina huduma mbili kama ifuatavyo:

    i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu

    ii. Udhibiti wa ufuatiliaji na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii iliombewa **Shilingi Bilioni 11,205,996,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 417,096,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 2,788,900,000** ni ruzuku kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji

na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) ambapo **Shilingi Bilioni 1,864,900,00** Mishahara na **Shilingi Milioni 924,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Aidha, jumla ya **Shilingi Bilioni 8,000,000,000** zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

**27. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2025, Programu hii imepata jumla ya **Shilingi Bilioni 5,975,138,193** sawa na **asilimia 53.3**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Milioni 66,576,204** kwa matumizi ya Kawaida ya Uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi Bilioni 1,728,022,948** ni ruzuku kwa ZPRA na **Shilingi Bilioni 4,180,539,041** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU.

**28. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Utekelezaji wa ukondoishaji wa masuala ya Mpango makhsusi wa Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Planning) kupitia Idara ya Maendeleo ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu unaendelea kwa mashirikiano ya karibu na Ofisi ya Makamo wa Rais SMT.

Wizara tayari imeunda kamati ya watendaji kutoka katika taasisi mbali mbali za Serikali ambazo zinahusika na matumizi ya Bahari na wanaendelea kupatiwa mafunzo juu ya utekelezaji wa mpango huo. Pia watendaji ambao watahusika kuufanyia kazi mpango huu kutoka taasisi mbali mbali za Serikali wanaendelea kupatiwa mafunzo yanayoendelea kufadhiliwa na Serikali ya Sweden. Aidha, Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kufanya zoezi la majaribio la MSP katika eneo la Zone 5 katika hifadhi ya mkondo wa Pemba (PECCA).

ii. Idara imeratibu jumla ya mikutano tisa (9) ya washirika wa maendeleo juu ya kuendeleza zao la mwani pamoja na ujenzi wa madiko "Landing sites" na bandari ya Uvuvi.

iii. Idara imefanya mikutano kumi na nne (14) ya kutoa uelewa kuhusu Uchumi wa Buluu ndani na nje ya Zanzibar.

iv. Jumla ya mikutano 29 ya kikanda, kitaifa, na kimataifa imehudhuriwa kuhusiana na masuala ya Uchumi wa Buluu kwa lengo la kutangaza fursa za Uchumi wa Buluu zilizopo Zanzibar.

v. Idara imeratibu na kuzindua rasmi Jukwaa la Usimamizi wa Urithi na Uhifadhi wa Bahari (Marine Heritage and Conservation Forum) ili wadau waweze kujadili masuala mbali mbali ya Uchumi wa Buluu.

vi. Idara imeendelea kutoa uelewa wa dhana ya Uchumi wa Buluu na vipaumbele vyake kwa umma, pamoja na wafanyakazi wa Taasisi mbali mbali za Serikali na sekta binafsi ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Tanga pamoja na Mtandao wa Wanahabari wa Kiafrika waliobobea katika Maendeleo Endelevu na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa 21).

vii. Idara kwa kupitia ufadhili wa UNDP imefanikiwa kuratibu na kutekeleza Mradi wa Bahari Maisha ambapo jumla ya vihori 150 vimetengenezwa na kugawiwa kwa wananchi wa Unguja, Pemba, Tanga na Bagamoyo. Kupitia Mradi huu, Taasisi ya Zanzibar Maishabora Foundation imefanikiwa kuwawezesha wakulima wa mwani pamoja na vijana zaidi ya 427 na kuwapatia elimu ya kifedha, kuvisajili vikundi vya mwani pamoja na kuvipatia vifaa.

**29. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu iliombewa **Shilingi Bilioni**

**11,205,996,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 417,096,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 2,788,900,000** ni ruzuku kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA). Aidha, jumla ya **Shilingi Bilioni 8,000,000,000** zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia. Hadi kufikia mwezi Machi 2025, Programu hii imepata jumla ya **Shilingi Bilioni 5,975,138,193** sawa na **asilimia 53.3**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Milioni 66,576,204** kwa matumizi ya Kawaida ya Uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi Bilioni 1,728,022,948** ni ruzuku kwa ZPRA na **Shilingi Bilioni 4,180,539,041** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA (ZPRA)**

30. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

31. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Mamlaka ilifanya tathmini ya kitaalamu katika eneo lililokuwa kitalu cha Pemba-Zanzibar na kuligawa katika vitalu viwili (2) vipya kwa ajili ya uwekezaji. Vitalu hivyo vimepewa majina ya Z1 na Z2. Hatua hiyo imepelekea Zanzibar kuwa na vitalu 10 kwa ajili ya uwekezaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeridhia mpango wa utoaji wa vitalu husika kwa njia ya moja kwa moja (direct awarding) ikiwa ni mbinu ya kurahisisha upatikanaji wa Kampuni itakayoingia makubaliano na Serikali.

ii. Mamlaka imeshiriki Majukwaa Saba (7) ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi Asilia kwa ajili ya Kutangaza Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia kwa Wawekezaji wa Kimataifa. Muamko wa Makampuni hayo kuja kuwekeza Zanzibar ni mkubwa ambapo wizara inaendelea na majadiliano na baadhi ya wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuja kuwekeza Zanzibar.

iii. Mamlaka imeratibu uingiaji wa Mkataba baina ya Kampuni ya RAKGas, ZPDC na Wizara mnamo mwezi Machi 2025, kwa ajili ya uhaulishaji wa fedha za madai mia saba na hamsini na tisa (759) ya fidia iliyobaki kulipwa kwa Wananchi walioathirika na zoezi

la mtetemo lililofanywa katika eneo la kitalu cha Pemba-Zanzibar na Kampuni ya RAKGas.

iv. Mamlaka imefanikiwa kukamilisha uanzishwaji wa kituo cha muda cha kuhifadhia na kusimamia taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) kwa kujenga chumba cha kukagulia taarifa, kununua vifaa, software na kufanya mafunzo kwa wataalamu wa Mamlaka katika matumizi ya vifaa na software hizo ((Kiambatisho Nam. 10a).

v. Mamlaka imeendesha jumla ya programu 17 za kujenga uelewa kuhusiana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na gesi asilia Zanzibar kupitia mikutano ya Taasisi, wananchi wa shehia mbalimbali pamoja na vipindi vya redio na Televisheni.

vi. Mamlaka imeingia mkataba na Kampuni ya Geopartners ya Uingereza kwa ajili ya kufanya utafiti wa maeneo yanayovuja mafuta na gesi asilia katika maeneo ya kina kirefu ya bahari ya Zanzibar.

vii. Mamlaka imekamilisha mazungumzo na Kampuni ya SLB kwa ajili ya kuchukua taarifa mpya za mtetemo katika maeneo ya kina kirefu ya bahari ya Zanzibar. Mkataba wa uchukuaji taarifa hizo umesainiwa mwezi Aprili, 2025 nchini Uingereza.

viii. Mamlaka imefanikiwa kutoa jumla ya Mafunzo kumi na mbili (12) kwa watendaji wake yakiwemo tisa (9) ya muda mfupi, mawili (2) ya vitendo na moja (1) ya muda mrefu yanayolenga kuimarisha uwezo wa usimamizi na udhibiti wa shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 6,788,900,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,864,900,000** ni Mishahara, **Shilingi Milioni 924,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 4,000,000,0000** ni kwa kutekeleza mradi wa maendeleo (NDR). Hadi kufikia Machi 2025, Mamlaka imepatiwa **Shilingi Bilioni 3,636,091,989** sawa na **asilimia 54**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,328,565,694** ni Mishahara, **Shilingi Milioni 399,457,254** ni matumizi ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi Bilioni 1,908,069,041** kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo wa NDR.

## KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPDC).

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imelenga

kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kampuni imeanza kufanya Upembuzi Yakinifu (feasibility study) kwa lengo la kupata tathmini ya kutosha kwa utekelezaji wa mradi pamoja na uendeshaji wa biashara ya mafuta na Bohari ((Kiambatisho Nam. 10b). Aidha, Kampuni inaendelea kufanya mazungumzo na Kampuni binafsi ya Mafuta na Gesi kwa lengo la Mashirikiano katika ujenzi wa Bohari ya Mafuta pamoja na biashara ya Mafuta Zanzibar.

ii. Kampuni imetoa Mafunzo ya Muda Mrefu ya Mafuta na Gesi kwa Mfanyakazi mmoja (1) katika ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Jiolojia. Aidha, Kampuni imetoa Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Wafanyakazi 16 kwa fani mbali mbali.

iii. ZPDC ilishiriki katika duru ya kwanza ya utowaji wa leseni kwa vitalu nane (8) vya Baharini, utoaji wa mafunzo ya uandaaji wa financial and economic model kwa Wafanyakazi 10 sambamba na utayarishaji wa Model hiyo, ambao ulifanyika kwa lengo

la kutathmini uwekezaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa mkondo wa juu. Aidha, Kampuni ilishiriki katika utangazaji wa duru ya kwanza ya utowaji wa vitalu vya Baharini nchini Uingereza na Afrika ya Kusini.

iv. Kampuni imetoa uelewa juu ya Mafuta na Gesi Asilia kwa wananchi kupitia Gazeti la Zanzibar Leo na Televisheni pamoja na kushiriki Makongamano 6 ya Mafuta na Gesi ndani na nje ya Nchi.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 4,000,000,000** kwa kutekeleza mradi wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, Wizara ilipatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 2,272,470,000** sawa na **asilimia 56.8** kwa ajili ya ufunguzi na tathmini ya duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari;

36. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 51,089,282,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 4,061,516,000** ni kwa matumizi ya kawaida ambapo, **Shilingi Bilioni 1,744,212,000** ni Mishahara, **Shilingi Milioni 752,804,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi, na **Shilingi Bilioni 1,564,500,000** ni ruzuku kwa ajili ya ZAFIRI na ZAFICO. Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 47,027,766,000**. Kati ya hizo **Shilingi Bilioni 31,000,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 16,027,766,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

37. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025 programu hii imepata jumla ya **Shilingi Bilioni 20,594,999,842** sawa na **asilimia 40.3.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 2,381,920,284** kwa Matumizi ya kawaida. Ambapo **Shilingi Bilioni 1,237,067,215** Mishahara, **Shilingi Milioni 180,064,673** kwa ajili ya Matumizi Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Milioni 964,788,396** ni ruzuku. Katika kutekeleza miradi ya Maendeleo Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni**

**18,213,079,558** ambapo **Shilingi Bilioni 16,865,089,296** kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 1,347,990,262** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

**38. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu ndogo hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Wakulima wa mwani 1,602 wamepatiwa vifaa vya kilimo cha mwani ikiwemo taitai bunda 2,350 na Kamba bunda 3,959. Wakulima waliofaidika ni kutoka shehia za Makunduchi, Bweleo, Uroa, Pongwe, Tumbatu Gomani na Marumbi. Aidha vihori 87 (Unguja 29 na Pemba 58) vya kubebea mwani vimegawiwa kwa wakulima wa shehia za Muungoni kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wakati wa uvunaji wa mwani wao.

ii. Wakulima wa mwani 3,100 wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za kilimo cha mwani katika shehia za Jambiani kikadini, Jambiani kibigija, Tumbatu Gomani, Kidoti,

Fukuchani, Kisakasaka, Uzi, Ng'ambwa na Dimani kwa unguja na kwa Pemba ni Tumbe Mashariki, Tumbe Magharibi, Shumba Mjini, Fundo, Gando na Shanake. Aidha jumla ya mashamba darasa matano (5) yameanzishwa katika shehia za Pete, Muyuni A, Jambiani kibigija, Unguja Ukuu na Marumbi.

iii. Ziara 12 za uhakiki wa wakulima wa mwani katika shehia 46 kati ya 51 za Unguja zimefanyika kwa lengo la kutambua idadi ya wakulima wa mwani waliokuwepo kwenye shehia hizo. Miongoni mwa shehia hizo ni pamoja na Uroa, Tumbatu (Gomani, Uvivini na Jongowe), Uzi, Ngambwa, Unguja Ukuu, Kikungwi, Pongwe, Chwaka, Marumbi, Michamvi, Bwejuu, Paje, Jambiani (Kikadini na Kibigija), Muungoni, Pete, Muyuni A na B, Ukongoroni, Makunduchi (Kijini, Tasani, Kajengwa, Mzuri, Kiongoni na Mtende), Pwani Mchangani, Kiwengwa, Kijini Matemwe, Kilindi, Kigunda,Tazari, Kilimani, Kidoti, Fukuchani, Potoa, Muange, Buyu, Fuoni Kibondeni, Bungi, Nyamanzi, Kisakasaka, Bweleo, Dimani na Pitanazako. Aidha Zoezi la uchambuzi wa idadi halisi ya wakulima litanyika pale zoezi zima la uhakiki litakapokamilika.

iv. Kupitia Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi na Chuo cha Mipango cha Mwanza makaushio manne ya kukaushia mwani (Solar Drier) yamejengwa katika Shehia ya Uzi, Muungoni na Kiuyu Mbuyuni. Vile vile, mashine mbili za kusagia mwani zimegawiwa kwa wakulima wa Shehia ya Kiuyu Pemba na Pwani Mchangani Unguja. Aidha, jumla ya chanja 140 za kuanikia mwani zimejengwa katika shehia ya Muungoni Unguja na Kiuyu Pemba.

v. Kupitia mradi wa WorldFish Jumla ya wavuvi 100 na wakuu wa madiko 30 wamepatiwa mafunzo kuhusu mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za uvuvi kupitia vifaa maalumu vya PDS. Aidha, PDS 100 zimefungwa kwenye vyombo 100 vya uvuvi Unguja na Pemba ambapo 60 Unguja na 40 Pemba.

vi. Kuanzishwa kwa Mfumo wa usajili wa wavuvi na utoaji wa leseni kwa njia ya kieletroniki hivyo kuwafanya wavuvi kusajiliwa na kupatiwa leseni kupitia mfumo huu moja kwa moja. Katika kuimarisha uchukuaji wa takwimu za samaki mizani 10 za kupimia uzito wa samaki zimegawiwa katika madiko 10 ya Wilaya ya Kaskazini A. Pia, jumla ya vishikwambi 30 vimetolewa kwa wakuu wa madiko ili kurahisisha ukusanyaji wa takwimu za uvuvi Unguja na Pemba ambapo Unguja 18 na Pemba 12.

vii. Katika kuimarisha miundombinu ya masoko na madiko ya kisasa Idara inaendelea na usimamizi wa ujenzi wa madiko na masoko mawili ya samaki ya kisasa katika eneo la Mkoani kwa Pemba (**Kiambatisho Nam. 10c**) na Fungurefu kwa Unguja (**Kiambatisho Nam. 10d**).

viii. Katika kuimarisha ufugaji wa majongoo bahari na upatikanaji wa vifaranga vya majongoo, Idara kwa kushirikiana na Kampuni ya Zanzibar marine Hatchery imezalisha jumla na vifaranga 1,500,000, kati ya hivyo vifaranga 80,000 vimegawiwa kwa wafugaji Unguja na Pemba na vifaranga 70,000 kwa ajili ya biashara na uzalishaji wa hatchery.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 50,745,946,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 3,718,180,000** kwa matumizi ya kawaida, ambapo **Shilingi Bilioni 1,744,212,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 409,468,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 1,564,500,000** ni Ruzuku. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 47,027,766,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 31,000,000,000** ni kutoka SMZ na

**Shilingi Bilioni 16,027,766,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

40. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025 programu ndogo hii imepata jumla ya **Shilingi Bilioni 20,508,321,882** sawa na **asilimia 40.4**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 2,295,242,324** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi Bilioni 1,237,067,215** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 93,386,713** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi Milioni 964,788,396** ni ruzuku. Katika kutekeleza miradi ya Maendeleo Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 18,213,079,558** ambapo **Shilingi Bilioni 16,865,089,296** kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 1,347,990,262** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR - ZAFIRI

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Malisili za Baharini Zanzibar imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Taasisi imefanikiwa kufanya jumla ya tafiti tano (5) ikiwemo utafiti wa ukadiriaji wa kiwango cha uzalishaji wa taka zinazotokana na samaki na uwezekano wa kutumika kwa taka hizo kutengeneza chakula cha Mifugo,

Utafiti ya mchango wa kijamii na kiuchumi wa Uvuvi wa kuokota (Uvuvi wa jamii za Chaza), Utafiti wa kuangalia Ubora wa maji ya Bahari na Fukwe za Zanzibar, Utafiti wa Mbegu za mwani zinazolimwa na kupatikana Zanzibar na Utafiti wa kuangalia maandiko mbali mbali (review) yanayohusu Sumuasili katika Kasa. Ripoti za tafiti hizo tayari zimekamilika kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wadau mbali mbali wa Uvuvi nchini.

ii. Taasisi imefanikiwa kuboresha Miundombinu ya Maabaraa kufuatia ununuzi wa vifaa vipya na vya kisasa katika Maabara za Microbiolojia na Kemia kwa ajili ya uchambuzi wa taarifa/sampuli za kitafiti pamoja na uthaminishaji wa bidhaa za Uvuvi na ufugaji wa viumbe maji ambazo zinahitaji kusafirishwa nje ya nchi (**(Kiambatisho Nam. 10e**).

iii. Taasisi imefanikiwa kujenga uzio kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa Jengo la Taasisi pamoja na kukidhi viwango vya kuwa na Maabara bora zinazokubalika.

iv. Taasisi imefanikiwa kuweka vifaa vya kufuatilia mienendo ya bahari ikiwemo vifaa vya kupima kujaa na kupwa kwa maji ya bahari (Tide Gauges), vifaa vya kupima tabia za bahari kama vile joto la bahari, mikondo

ya bahari n.k. Vifaa hivyo ni pamoja na Boya na Sediment trap.

v. Taasisi kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi imefanikiwa kufunga vifaa vya Pelagic data System (PDS) na kuweka mfumo wa utambuzi wa mienendo ya Boti 100 za Uvuvi Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha usimamizi bora wa sekta ya uvuvi.

vi. Taasisi imefanikiwa kuanzisha Bodi ya Wakurugenzi kwa lengo la kuimarisha ufanisi na utendaji wa taasisi.

vii. Taasisi imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wawili (2) na wafanyakazi 24 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi yakiwemo matumizi ya mfumo (E-Office), uhasibu, Mfumo wa manunuzi, mafunzo ya matumizi ya mfumo wa rasilimali watu na malipo, mafunzo ya matumizi ya vifaa vya maabara na mafunzo ya uchambuzi wa taarifa za kisayansi.

viii. Taasisiimefanikiwakukamilishauanzishwaji wa maabara ya uzalishaji wa mbegu bora za mwani zenye kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika eneo la SUZA Beit- El Raas (Tissue Culture Laboratory) pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara hiyo kwa lengo la kuanza uzalishaji wa mbegu za mwani (**Kiambatisho Nam. 10f**).

ix. Taasisi imefanikiwa kushiriki katika utafiti wa ukusanyaji wa Taarifa za uvuvi (Samaki) katika ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi kupitia Programu ya Ecosystem Approach to Fisheries (EAF)-Nansen, ambapo watafiti wanne (4) walipanda katika Meli ya Utafiti ya Dr. Fridtjof Nansen katika bahari za Afrika ya Kusini, Mozambique na Tanzania.

x. Taasisi imesambaza matokeo ya tafiti za Uvuvi zilizofanyika kupitia maonesho mbali mbali yanaoyofanyika Zanzibar kama vile maonesho ya Nane Nane, maonesho ya Biashara, Kizimkazi Festival, Fahari ya Zanzibar na Mei Mosi.

**42. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 5,458,472,000**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,177,700,000** ni ruzuku kutoka SMZ ambapo **Shilingi Milioni 889,700,000** ni mishahara na **shilingi Milioni 288,000,000** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Aidha, **Shilingi Bilioni 4,280,772,000** kwa utekelezaji wa kazi za Maendeleo ambapo **Shilingi Bilioni 4,000,000,000** kutoka SMZ na **Shilingi Milioni 280,772,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025 Taasisi imepata jumla ya **Shilingi Bilioni 1,691,761,703**

sawa na **asilimia 30.9**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 585,957,545** ni Mishahara, **Shilingi Milioni 80,000,000** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 1,025,804,158** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi Milioni 728,472,242** kutoka SMZ na **Shilingi Milioni 297,331,916** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR – ZAFICO

43. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kampuni ya Uvuvi Zanzibar kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi imeendelea na hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mzabuni wa ununuzi wa meli kubwa ya uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Kampuni imeendelea na matayarisho ya kumtafuta mbia wa uendeshaji wa meli hiyo kwa mfumo wa PPP pamoja na Kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki (**Kiambatisho Nam. 10f**).

ii. Kampuni imekamalisha rasimu ya awali ya mchoro wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki na mitambo ya baridi kitakacho jengwa katika eneo la Fungurefu. Aidha, muwekezaji kutoka Afrika ya Kusini ameonesha nia ya kuwekeza katika

kiwanda hicho ambapo tayari amewasilisha pendekezo la andiko la mradi na mpango wa biashara, kwa sasa ZAFICO imewasiliana na Taasisi inayuhusiana na masuala ya ubia (PPP) kwa lengo la kupata ushauri wa kitaalamu.

iii. Katika kuimarisha mifumo ya baridi na uhifadhi wa samaki na mazao ya baharini, Kampuni ZAFICO imesimamia ujenzi wa chumba 1 cha baridi na sehemu ya usarifu na uhifadhi samaki Kizimkazi na ujenzi huo umekamilika. Aidha kwa sasa muekezaji mmoja ameonesha nia ya kufanya uwekezaji na amewasilisha nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya uwekezaji. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukaa na muwekezaji na kukamilisha taratibu za kisheria ili kuanza kuweka mifumo na mahitaji muhimu ya uendeshaji wa chumba hicho.

iv. ZAFICO inaendelea na Ujenzi wa miundombinu ya viwanda vya kusarifu dagaa KAMA - Unguja na Ndagoni – Pemba ambapo Utekelezaji miradi hii umefikia asilimia 65 kwa KAMA((Kiambatisho Nam. 10g) na asilimia 39 kwa Ndagoni (**Kiambatisho Nam. 10h**). Aidha, mara baada ya kukamilika miradi hii jumla ya wananchi 11,000 watanufaika Unguja na Pemba.

v. Rasimu ya awali ya muongozo wa uuzaji samaki imekamilika. Aidha, hatua za awali za kuandaa vigezo na mahitaji ya uuzaji wa samaki kwa lengo la kumlinda mlaji zimekamilika. Vile vile, vifaa vya uhifadhi wa samaki kama vile majokofu mawili (2) yamepatikana na kupelekwa Pemba kwa ajili ya kuhifadhi samaki na kurahisisha mauzo yenye tija.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO iliombewa jumla ya **Shilingi Milioni 386,800,000.** Hadi kufikia Machi 2025, Kampuni imepatiwa jumla ya **Shilingi Milioni 298,880,851** sawa na asilimia **77.2** ya fedha zilizopangwa.

## MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU - DSFA

45. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Mamlaka imetoa jumla ya leseni za uvuvi wa bahari kuu 38, vibali viwili (2) vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania (Areas beyond national jurisdiction), vibali vitano (5) vya uwakala wa meli, na leseni kwa meli mbili (2)

saidizi (supporting vessel). Aidha, Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Mamlaka ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 11,500,000,000**, hadi kufikia Machi 2025 jumla ya **Shilingi Bilioni 6,600,000,000** zimekusanywa sawa na **asilimia 57** ikilinganishwa na leseni 67 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kushuka kwa makusanyo kulitokana na kuanza kutumika kwa mfumo wa mgawanyo wa mavuno ya samaki aina ya Jodari Machomakubwa kupitia Kamisheni ya Jodari ya Bahari ya Hindi (IOTC) na kipindi cha makusanyo kuwa kifupi (Julai 2024 hadi Februari 2025). Hata hivyo, inatarajiwa kuwa mapato yataongezeka kutokana na kutoa leseni zaidi za meli za kuzungusha (Purse seines) kati ya Machi na Juni, 2025.

ii. Mamlaka imeendelea kukusanya takwimu za uvuvi wa samaki aina ya Jodari kila mwezi katika madiko saba (7) kwenye Wilaya za Mtwara mjini, Kilwa, Mafia, Nungwi, Wete, Kinondoni na Tanga mjini. Vile vile, Mamlaka imeendelea kukusanya takwimu za mavuno ya samaki kutoka kwenye meli zilizovua katika Ukanda Maalum wa Kiuchumi (EEZ) wa Tanzania na nje ya mipaka kwa meli za kitanzania kwa mujibu wa taratibu za IOTC. Meli za Kigeni zilizopewa leseni kuvua katika ukanda huo

ziliripoti kuvua kiasi cha Tani 7,647 na meli za Tanzania ziliripoti kuvua jumla ya tani 12,578 za samaki aina ya Jodari na jamii yake. Aidha, Mamlaka iliendelea kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kukamilisha mfumo wa kutambua maeneo yenye samaki wengi (Potential Fishing Zones - PFZ) ili kuwezesha kupata taarifa za masoko ya samaki kwa watumiaji.

iii. Katika kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za Uvuvi wa bahari kuu Mamlaka imekamilisha kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 3 Septemba, 2024. Maboresho hayo yanalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi wa uvuvi na kuimarisha masuala ya kiutendaji ya DSFA.

iv. Katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uvuvi wa bahari kuu na makubaliano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi kwenye bahari kuu, DSFA imeendelea kutumia mifumo ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli (Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification System – AIS) na kuweka Waangalizi wa Uvuvi

(Fishery Observers) kwenye meli zilizopewa leseni. Vile vile, DSFA ilifanya ukaguzi wa meli za uvuvi zilizoomba leseni na vibali katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar na Victoria - Ushelisheli. Aidha, DSFA kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (TNC) imekamilisha hatua za mwazo za matumizi ya mfumo wa kielekroniki (Electronic Monitoring System) ambao utahusisha kufunga kamera kwenye meli. Mfumo huo uitawezesha Serikali kuona shughuli za uvuvi wakati meli ikivua na kutaiwezesha Tanzania kutekeleza maazimio ya kikanda na kimataifa katika usimamizi wa meli hizo na ukusanyaji wa taarifa na takwimu sahihi na kwa wakati.

v. Mabaharia 14 wa Kitanzania (Tanzania bara - 7 na Zanzibar - 7) waliopewa mafunzo na ALBACORA Group waliendelea kufanya kazi katika meli za uvuvi wa kampuni hiyo.

## PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MALIASILI ZA BAHARI

**46. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Jumla ya Kamati za usimamizi shirikishi (21) za jamii zilijengewa uwezo wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira ya bahari na rasilimali zake ili kuimarisha mazingira na afya ya rasilimali za bahari kwa maslahi ya sekta ya uvuvi, ufugaji wa viumbe maji, ukulima wa mwani na utalii.

ii. Idara imeandaa muongozo na kutoa elimu kwa waongozaji watalii na waendesha boti za utalii juu ya namna bora ya kufanya utalii wa pomboo na utalii wa kiti cha pweza katika hifadhi ya MIMCA. Mabango 25 yenye ujumbe wa kuhifadhi viumbe adimu na waliohatarini kutoweka yaliwekwa katika maeneo yote ya Hifadhi ya Unguja na Pemba ili kuongeza uelewa miongoni mwa wavuvi na watumiaji wengine wa bahari.

iii. Jumla ya Doria shirikishi 183 zilifanyika katika maeneo yote ya hifadhi za bahari kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya pamoja na matumizi ya gesi). Wavuvi 382 walikamatwa wakijihusisha na makosa mbali mbali ambapo wengi wao walipatiwa elimu na kuachiwa na wachache walihukumiwa nje ya mahakama na kutozwa faini. Aidha, mafunzo ya doria kuhusu mbinu za ukamataji, jinsi ya kutoa huduma ya kwanza katika uokozi na kuanzisha mfumo wa

ufuatiliaji kwa viumbe walio hatarini kutoweka ili kuimarisha uhifadhi wa viumbe hao. Pia, boti 2 za Doria zimenunuliwa ili kudhibiti shughuli za uvuvi haramu katika maeneo ya Hifadhi na nje ya Hifadhi.

iv. Idara kwa kushirikiana na Taasisi ya Wildlife Conservation Socierty (WCS) imefanikiwa kukusanya maoni ya wanajamii na wavuvi wa shehia 25 za vijiji vyote vilivyopo mashariki ya Kisiwa cha Pemba pamoja na kuweka alama za mipaka katika eneo lililopendekezwa kwa kutumia teknologia ya "GPS" ili kuona uwezekano wa kuanzisha hifadhi mbili mpya upande wa mashariki ya Pemba.

v. Idara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo WCS ilifanya ufuatiliaji wa matumbawe katika eneo la TUMCA( hanga reef na mwana wa Mwana),MENAI (Kisiwa cha Pungume na Bawe) na PECCA (Misali, Matumbini na Kwata). Ufuatiliaji huo umebainisha kuwa matumbawe yameanza kujirudi pole pole baada ya kupauka kulikosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

vi. Matumbawe bandia 1,907 yamewekwa katika maeneo ya Hifadhi ya MIMCA (Uroa na Pongwe), TUMCA (Donge mwanda, Mto wa Pwani na Kiongwe), MBCA (Muyuni na Kizimkazi Mkunguni), PECCA (Msuka na Kukuu).

Matumbawe haya yanafanya kazi kubwa katika kurejesha afya ya bahari katika sehemu ambayo yanawekwa. Kazi hii imefanywa kwa mashirikiano na taasisi za WCS, &Beyond na MCCC (Mwambao).

vii. Idara inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbali mbali yanayotumia bahari hasa wavuvi na wadau wa utalii ili kuendelea na kuwa na bahari yenye afya inayozalisha samaki na kutoa mazingira bora kwa watalii. Kuongezeka samaki wanaovuliwa na kuongezeka idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu inaashiria mafanikio kwenye uhifadhi.

viii. Jumla ya wafanyakazi 9 (wanaume 4 na wanawake 5) walishiriki katika mafunzo ya usimamizi shirikishi wa rasilimali pamoja kubadilishana uzoefu juu ya kuendeleza shughuli za uhifadhi, na kujenga uhimilifu wa mabadiliko ya tabia nchi, Nchi zilizotembelewa ni Mozambique, Finland, Mombasa na Tanzania Bara (Tanga na Kilwa).

ix. Idara imeendelea kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo ili kuendeleza uhifadhi wa rasilimali za bahari na fukwe. Washirika hao ni IUCN, USAID Heshimu Bahari, WCS, MCCC Ltd, Blue Alliance,&Beyond na Blue Action Fund.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Programu ndogo hii imeombewa jumla ya **Shilingi Milioni 343,336,000** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2025, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi Milioni 86,677,960** sawa na **asilimia 25.3** ya fedha iliyopangwa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi wa sekta.Programu imegawika katika programu ndogo tatu nazo ni:

    i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

    ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti

    iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 3,717,488,000** kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 2,385,988,000** ni Mishahara na **Shilingi Bilioni 1,331,500,000** kwa matumizi

ya uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2025, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1,912,309,125** sawa na **asilimia 51.4.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,458,476,967** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 453,832,159** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Jumla ya Wafanyakazi 283 wamepatiwa stahiki zao, ikiwemo mishahara na posho za likizo.
ii. Jumla ya wafanyakazi 115 wamepatiwa mafunzo ambapo wafanyakazi 24 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao cheti 1, Digrii 6, Master 14 na Phd 3. Vile vile, wafanyakazi 91 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi katika fani Uchumi wa Buluu na uvuvi. Aidha,

wafanyakazi 11 wamepatiwa mafunzo ya awali (Induction Course) Unguja na Pemba.

iii. Jumla ya wafanyakazi wapya 11 wameajiriwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kupangiwa kazi katika taasisi mbali mbali za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Vile vile, wafanyakazi 13 tayari wamethibishwa kazi.

iv. Kuimarisha Miundombinu ya Mawasiliano ikiwa ni pamoja na ufungaji wa vifaa vya kisasa vya Mawasiliano, Mifumo ya kuhifadhi na Usambazaji wa taarifa kwa njia ya kidijitali ili kuongeza kasi na udhibiti wa mtandao.

v. Hatua za udhibiti wa mali za Serikali ziliendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa na kuwasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mali hizo chakavu zimeshafanyiwa uhakiki hivi sasa zinasubiwa kufanyiwa tathmini kwa hatua zinazofaa.

vi. Taarifa zinzohusiana na Uchumi wa Buluu na Uvuvi zimeendelea kutolewa kwa jamii kupitia vyombo mbali mbali vya habari ikiwemo vipindi 5 vya Televisheni na redio, Mikutano 3 ya waandishi wa habari, Makala 3 za TV na Redio, majarida 3 pamoja na kutoa taarifa 80 katika mitandao ya kijamii ya facebook, Twitter na Instagram.

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, imeombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 2,004,294,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,233,899,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 770,395,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2025 Programu ndogo hii imepatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1,092,052,160** sawa na **asilimia 54.5.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 748,391,262** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi Milioni 343,660,898** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

53. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

   i. Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT) katika kusajili na hatimae kuruhusu usafirishaji wa mwani na mazao mengine ya baharini kutoka Zanzibar moja kwa moja kwenda katika soko la China ambapo hadi sasa makampuni 12 yamesajiliwa.

ii. Kuwasilisha Waraka wa Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 na kutunga Sheria ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa bahari katika kikao cha Makatibu Wakuu na Kikao cha Baraza la Mapinduzi;

iii. Kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji wa Takwimu za ajira zilizozalishwa kuanzia Oktoba 2023 hadi Novemba 2024 katika sekta ya Uchumi wa Buluu ili kutathmini utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 13 (b) la kuzalisha ajira 300,000 ifikapo 2025.

iv. Kuwasilisha Ripoti ya mwaka ya Takwimu za sekta ya uvuvi kwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

v. Kushiriki katika mchakato wa Tanzania wa kuripoti utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za binadamu.

vi. Kushiriki katika vikao vya Tume za Pamoja za Ushirikiano (JPC) na nchi mbali mbali. Kushiriki katika kikao cha mashirikiano kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania Bara na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vii. Kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo na kuziwasilisha katika Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango kwa mwaka 2024/2025 imeombewa jumla ya **Shilingi Milioni 493,145,000**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Milioni 140,982,000** ni Mishahara, na **Shilingi Milioni 352,163,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufika Machi 2025, Proramu ndogo hii imepatiwa jumla ya **Shilingi Milioni 171,431,797** sawa na **asilimia 34.8.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi Milioni 117,288,077** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 54,143,720** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA.

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu utekelezaji wa kazi za mipango ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa upande wa Pemba.

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu Vikao vitatu (3) vya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi; na kutembelea miradi mbali mbali ya ujenzi wa Miundombinu ikiwemo; Ujenzi wa Diko na soko la Kisasa la samaki Mkoani, Kiwanda cha Kusarifu Dagaa Ndagoni pamoja na Wanufaika wa Programu ya UVIKO 19.

ii. Kuratibu ziara nne (4) za Viongozi wa Wizara na Kitaifa. Kupitia ziara hizo Maagizo mbali mbali yalitolewa ikiwemo ujenzi wa vidaraja katika Kisiwa cha Kokota kwa ajili ya Wakulima wa Mwani na Uvuvi, ambao kwa sasa ujenzi huo umekamilika na ujenzi wa soko la Kiwani ambapo utekelezaji wake upo katika hatua ya ufungaji wa Mkataba.

iii. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara ikiwemo Idara na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba.

iv. Aidha, jumla ya vikao vinne (4) vya Wadau wa Uchumi wa Buluu wakiwemo wavuvi na wakulima wa mwani kutoka Shehia mbali mbali vimefanyika, kwa lengo la kushajihisha matumizi bora ya maeneo ya uhifadhi ikiwa

ni pamoja na matumizi ya zana sahihi za uvuvi ili kulinda rasilimali za bahari.

v. Wizara kwa kushirikiana na IUCN imezifikia Shehia 33 zilizopo ndani ya ukanda wa PECCA kwa lengo la kuhamasisha wanajamii juu ya Uanzishwaji wa Hifadhi mpya maeneo ya Kaskazini na Kusini Mashariki ya Pemba.

vi. Wizara kupitia Divisheni ya Mipango imefanikiwa kufanya Utafiti mdogo uliolenga kutathmini athari iliyopatikana kwa Wavuvi na Wakulima wa mwani waliopatiwa Mkopo wa Boti kupitia Mradi wa Ahueni UVIKO 19 katika kijiji cha Tumbe Mashariki na Tumbe Magharibi. Aidha, Matokeo ya Utafiti yalionyesha kwamba, asilimia 69.2 ya Wanufaika wameeleza kwamba mikopo imewanufaisha na kuongeza ajira kwa Vijana, Wanawake na jamii kwa ujumla na kuboresha shughuli zao za Kiuchumi zinazohusiana na Uchumi wa Buluu na shughuli nyengine za Kiuchumi na Kijamii.

vii. Katika jitihada za kupunguza uvuvi haramu, kupitia mfumo wa Gear Mbadala, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Blue Allience, imegawa Madema 100 na Mishipi 35 kwa Wavuvi 40 ambao walikamatwa wakijihusisha na uvuvi haramu.

viii. Wizara imefanya vikao vinne (4) na Wadau wa Maendeleo wakiwemo; IUCN, Mwambao, TNC, Tanga Pemba – Sea Scape kwa ajili ya Kuhamasisha masuala ya Uhifadhi wa maeneo ya Bahari na shughuli nyengine zinazohusiana na Uchumi wa Buluu. Aidha, kupitia Washirika wa Maendeleo, jumla ya Shilingi Milioni 480 zimetolewa kwa Vikundi 15, ambapo kila Kikundi kilipatiwa Milioni 32 kwa ajili ya kuimarisha shughuli zao za Uchumi wa Buluu.

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Programu hii imeombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 1,220,049,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,011,107,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 208,942,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2025, Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi Milioni 648,825,168** sawa na **asilimia 53.2.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 592,797,628** ni mishahara na **Shilingi Milioni 56,027,541** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

## CHANGAMOTO

58. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitahada za Wizara na Serikali kwa ujumla, Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

| Nam | Changamoto | Hatua zilizochukuliwa |
|---|---|---|
| 1. | Kuwepo matukio ya Uvuvi Haramu na Mabadiliko ya Tabia nchi. | Kazi ya utoaji wa elimu pamoja na doria zinaendelea kufanyika ikiwemo kuimarisha misingi mipya ya Sera na Sheria. Pia, Wizara inaendelea na utoaji wa elimu juu ya mabadiliko ya tabia nchi na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uvuvi ambazo ni rafiki kwa mazingira ikiwa ni pamoja na kuendeleza sekta ya ufugaji wa mazao ya baharini. |
| 2. | Uhaba wa teknolojia na vifaa vya kutendea kazi | Wizara imeendelea kupokea vifaa vya ofisi kupitia SMZ na washirika wa Maendeleo. Wizara inaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuhakikisha inakuwa na teknolojia bora itakayorahisisha utendaji wa kazi za wizara. |

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## MAKADIRIO YA MAPATO 2025/2026

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi Bilioni 11,273,214,000** kutoka vianzio vyake 5 vya Unguja na Pemba (**Kiambatisho Namb. 5**).

## MAKADIRIO YA MATUMIZI 2025/2026

**60.** **Mheshimiwa Spika**, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 172,033,961,377.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 14,952,100,000**

kwa Kazi za Kawaida na **Shilingi Bilioni 157,081,861,377** kwa Kazi za Maendeleo. (**Kiambatisho Namb. 6**).

61. **Mheshimiwa Spika,** mgawanyiko wa fedha za kawaida ni **Shilingi Bilioni 14,952,100,000.** Kati ya hizo, **Shilingi Bilioni 4,404,900,000** ni Mishahara, **Shilingi Bilioni 5,926,500,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 4,620,700,000** ni ruzuku kutoka SMZ. Kwa fedha za ruzuku, **Shilingi Bilioni 3,050,800,000** kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), **Shilingi Bilioni 1,140,500,000** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) na **Shilingi Milioni 429,400,000** kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO). (**Kiambatisho Namb. 6**).

62. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 157,081,861,377** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 131,245,370,000** SMZ na **Shilingi Bilioni 25,836,491,377** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambapo **Shilingi Bilioni 23,138,491,377** ni Mkopo na **Shilingi Bilioni 2,698,000,000** ni ruzuku (**Kiambatisho Namb. 7**). Aidha, jumla ya **Shilingi Bilioni**

**3,000,000,000** zimetengwa kupitia bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC).

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 itatekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tatu na Programu ndogo saba(7) ambazo ni:

i. Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;

- Programu Ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu
- Programu Ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

ii. Programu Kuuya Maendeleo ya Uvuvi;

- Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini.
- Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari.

iii. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

- Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.
- Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.
- Programu Ndogo ya Kazi za Uchumi wa Buluu Pemba.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara itatekeleza Miradi ya Maendeleo kumi (10) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 157,081,861,377** ifuatavyo:

i. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba.

ii. Ujenzi wa viwanda vya kusarifu na uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini.

iii. Mradi wa ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki.

iv. Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi unaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) ikiwemo ununuzi wa meli kubwa ya uvuvi wa Bahari Kuu.

v. Mradi wa kukuza usimamizi endelevu wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji wa bahari (TASFAM).

vi. Seaweed social enterprise program (SESEP).

vii. Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini unaofadhiliwa na Shirika la KOICA.

viii. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Taifa cha kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR).

ix. Mradi wa usambazaji wa Gesi Zanzibar.

x. Mradi wa Utafiti wenye lengo la Kudumisha Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii.

65. **Mheshimiwa Spika,** Aidha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 itatekeleza jumla ya miradi mengine mitano (5) kwa mashirikiano na Taasisi zisizo za Serikali (NGO's) kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Bahari Mali unaofadhiliwa na Ubalozi wa Jamhuri ya Ireland wenye thamani ya Euro 1.8 Milioni.

ii. Mradi wa Bahari ni Urithi unaotekelezwa na Shirika la WCS kupitia mfuko wa "Blue Action Fund" wenye thamani ya Euro 5.8 Milioni.

iii. Mradi wa Usimamizi wa Kijamii wa Maeneo ya Kiikolojia ya Bahari unaotekelezwa na Shirika la Mwambao kupitia "Blue Action Fund". Mradi huu unagharimu Euro Laki 327,927.67.

iv. Mradi wa Bahari Yetu unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (Europian Union). Mradi huu unagharimu Euro 1.1 Milioni.

v. Mradi wa Uhifadhi wa "North West Conservation" unaofadhiliwa na Shirika la Blue Alliance wenye thamani ya US$ 2.2 Milioni.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 itaendelea na uwezeshaji wa jamii kupitia Programu ya uwezeshaji wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi "Blue Economy Intervention Plan".

## MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2025/2026

67. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar (2022), kwa kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari na kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi kuhusiana na fursa za Uchumi wa Buluu ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko pamoja na kuchangia katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, mwani, uhifadhi wa bahari, utafiti wa uvuvi na bahari, biashara za baharini,

utalii, mafuta na gesi asilia pamoja na nishati mbadala.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i. Utoaji wa elimu na uelewa katika masuala ya Uchumi wa Buluu ikiwemo mbinu, nyenzo, mitaji na utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla.

ii. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Uvuvi Endelevu wa Mwambao na Bahari Kuu.

iii. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Kilimo cha Mwani.

iv. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Ufugaji wa Viumbe Maji (Majongoo Bahari, Kaa na Samaki).

v. Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Nishati Mbadala za Baharini.

vi. Ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi pamoja na biashara ya Mafuta na Gesi.

vii. Ujenzi wa Miundombinu ya Bandari za uvuvi, Madiko, Masoko, Viwanda, Huduma na Biashara za Uchumi wa Mazao ya Baharini.

viii. Utafiti wa Uvuvi, Sayansi za Bahari, Maliasili za Bahari, Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi Baharini.

ix. Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (Matumbawe, Nyasi Bahari, Mikoko na Bioanuwai ya Baharini).

x. Utalii Endelevu wa Mwambao na Bahari.

xi. Usimamizi wa Bahari (Usalama wa Bahari, Kuimarisha Ulinzi wa Bahari na Kupambana na Uvuvi Haramu Usioripotiwa).

xii. Kuweka misingi imara na kuimarisha utekelezaji wa bajeti inayozingatia jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**69. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imegawika katika Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Programu ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia

**70. Mheshimiwa Spika**, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 26,740,300,000** kwa ajili ya Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Kati ya fedha

hizo **Shilingi Bilioni 4,165,300,000** kwa Kazi za Kawaida na **Shilingi Bilioni 22,575,000,000** kwa Kazi za Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**71. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu sekta za kipaumbele za Uchumi wa Buluu;

ii. Kuhamasisha na kujenga uwezo kwa jamii kuhusu Uchumi wa Buluu;

iii. Kuratibu Masuala ya Uwezeshaji na Uongezaji wa Thamani wa Mazao ya Baharini na upatikanaji wa Masoko;

iv. Kuendeleza, kuwezesha, kutekeleza, kufuatilia na kuratibu MSP- Zanzibar;

v. Kuratibu ushiriki wa kitaifa, kikanda na Kimataifa katika shughuli za Uchumi wa Buluu; na

vi. Kuratibu utambuzi wa mahitaji ya kuandaa na kusimamia “Dashboard” ya Uchumi wa Buluu na “Satellite Account”.

72. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 7,201,500,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Milioni 200,000,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Milioni 426,500,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 6,575,000,000** kutoka SMZ kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

73. **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inajukumu la kusimamia Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuandaa na kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria kwa kuendesha tathmini ya utekelezaji wa Sera, kukamilisha marekebisho ya Sheria mpya pamoja na kufanyia mapitio ya Kanuni mbili za Sheria

kwa lengo la Usimamizi bora wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

ii. Kuratibu zoezi la utangazaji wa fursa za uwekezaji wa Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia na kusimamia majadiliano na wawekezaji kwa ajili ya shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

iii. Kuhamasisha ushiriki wa wazawa katika fursa zinazotokana na uwekezaji wa shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar kwa kuendesha mikutano na wananchi na wadau mbali mbali wa Sekta pamoja na kujengea uwezo Taasisi.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 19,538,800,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 3,538,800,000** kwa Kazi za Kawaida ambapo **Shilingi Milioni 90,000,000** ni Mishahara, **Shilingi Milioni 398,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 3,050,800,000** ni ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA). Katika kutelekeza Miradi ya Maendeleo Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 16,000,000,000**.

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA).

75. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kuendeleza majukumu yake ya kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ZPRAinalenga kutekeleza shabaha zifutazo;

i. Kuendelea kutangaza vitalu kumi (10) ili kuvipatia wawekezaji wa kuviendeleza kwa ajili ya shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kupitia majukwaa mbali mbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kusimamia utekelezaji wake.

ii. Kushirikiana na Kampuni ya SLB na Geopartners kwa ajili ya kukusanya taarifa za ziada za Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo ya Zanzibar.

iii. Kuendeleza mashirikiano na wadau mbali mbali wa ndani na nje wa sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

iv. Kuendelea kutekeleza mradi wa NDR kwa hatua ya Ujenzi wa kituo cha kudumu cha kuhifadhia taarifa za Mafuta na Gesi Asilia.

v. Kusimamia ukamilishaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na zoezi la mtetemo.

vi. Kuendesha Programu za kukuza uelewa kwa wananchi kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia kupitia mikutano ya hadhara katika shehia, mikutano ya Taasisi, makongamano pamoja na vyombo vya Habari.

vii. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Mamlaka ikiwemo ubora wa ofisi, nguvu kazi na maslahi ya watendaji pamoja na kuwajengea uwezo waliopo ili kuchochea uwajibikaji wao na kuongeza ufanisi.

**76. Mheshimiwa Spika,** naliomba baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 10,050,800,000** kwa ajili ya Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA). Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,942,100,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni 1,108,700,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 7,000,000,000** kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo.

## KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR, ZPDC

**77. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inalenga

kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kushiriki katika Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kama Kampuni ya Kibiashara ya Serikali.

ii. Kujenga Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia kwa matumizi ya Majumbani, Sehemu za kibiashara na vyombo vya usafiri.

iii. Kuendesha Programu za kujenga uelewa kwa Wananchi kuhusiana na ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Taasisi za Kibiashara na Majumbani.

iv. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Wafanyakazi ikiwemo kuwajengea uwezo kwa Watendaji wa Kampuni.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 9,000,000,000** kwa ajili ya Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar kutoka SMZ kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

79. **Mheshimiwa Spikai,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Baharini.

80. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 141,628,761,377** kwa ajili ya Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi. Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 7,121,900,000** kwa Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni 134,506,861,377** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi Bilioni 108,670,370,000** kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 25,836,491,377** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

81. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza Uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuimarisha kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji wa mwani kutoka tani 19,715 hadi tani 30,000 kwa kuwapatia wakulima elimu na vifaa vya kisasa vya kilimo.

ii. Kuongeza kiwango cha Samaki wanaovuliwa kutoka tani 78,943 hadi tani 115,000.

iii. Kuongeza uzalishaji wa Samaki wanaofugwa kutoka tani 3.5 hadi kufikia tani 6.

iv. Kuengeza usafirishaji wa mazao ya baharini yanayosafirishwa nje ya nchi kutoka tani 14,626 hadi kufikia tani 30,000

v. Kuendelea na zoezi la Usajili na utoaji wa lesseni za kielektroniki kwa wavuvi 5,000.

vi. Kukamilisha ujenzi wa Madiko na Masoko ya Samaki ya Mkoani Pemba na Fungurefu-Mkokotoni Unguja na kujenga Madiko na Masoko mapya mawili makubwa na 5 madogo Unguja na Pemba.

vii. Kuanza Ujenzi wa Kituo cha usarifu wa Mwani Makunduchi.

viii. Kuanza mchakato wa kuanzisha Chuo cha Uvuvi Shumba Mjini Pemba.

82. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya

**Shilingi Bilioni 137,928,761,377** kwa ajili ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 3,421,900,000** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi Bilioni 1,100,000,000** Mishahara, **Shilingi Milioni 752,000,000** Matumizi ya Uendeshaji ya Ofisi na **Shilingi Bilioni 1,569,900,000** ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO). Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi Bilioni 134,506,861,377**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 108,670,370,000** kutoka SMZ na **Shilingi Bilioni 25,836,491,377** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR (ZAFIRI)

83. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza tafiti za kuimarisha Sekta ya Uvuvi.

ii. Ukuzaji wa Teknolojia kwa Uvuvi mdogo mdogo.

iii. Kuimarisha Upatikanaji wa mbegu bora za Mwani.

iv. Kuongeza Wigo katika Ukuzaji na Ufugaji wa Viumbe maji.

v. Kuendeleza tafiti za kuimarisha uhifadhi wa mazingira ya bahari.

vi. Kuimarisha miundombinu ya maabara za microbiolojia na kemia.

vii. Kukuza mashirikiano na Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi.

**84. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 1,153,500,000** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI). Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 794,900,000** Mishahara, **Shilingi Milioni 345,600,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Milioni 13,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa utekelezaji wa kazi za Maendeleo.

## KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR - ZAFICO

**85. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa meli ya uvuvi wa bahari Kuu pamoja na kumtafuta mbia atakaeweza kuendesha meli hiyo kwa njia ya PPP kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - IFAD.

ii. Kuanza ujenzi wa Kiwanda Jumuishi cha kuchakata samaki na mitambo ya baridi Fungurefu- Mkokotoni.

iii. Kuwawezesha wajasiriamali wa dagaa kuongeza thamani na ubora wa dagaa kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kuongeza thamani na ubora wa dagaa wa Zanzibar Ndagoni na KAMA.

86. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 51,429,400,000** kutoka SMZ kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ambapo **Shilingi Milioni 429,400,000** ni ruzuku ya Mishahara na **Shilingi Bilioni 51,000,000,000** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

## MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU -DSFA

87. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutoa leseni, vibali na tozo kwa meli za Uvuvi wa Bahari kuu 89 kutoka ndani na nje ya nchi na vyanzo vyengine ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 11.8 zitakusanywa.

ii. DSFA kwa kushirikiana na ALBACORA Group itaendelea kutekeleza makubaliano ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki katika Manispaa ya Tanga, kushusha tani 100 za samaki wasiolengwa, na kujenga uwezo wa mabaharia wa Kitanzania katika uvuvi wa bahari kuu.

iii. Serikali kupitia DSFA itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu vivutio na fursa zinazopatikana kwenye uvuvi wa bahari kuu na kuimarisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu na kufanya mazungumzo na wawekezaji ili kuchagiza uchukuaji wa leseni na uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya bandari na viwanda vya samaki.

iv. Kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari kwa kuweka Waangalizi wa Uvuvi, kufanya ukaguzi wa meli na kufanya doria za kwenye maji na anga kwa mashirikiano na Jumuiya za Kikanda.

v. DSFA itaanza ufuatiliaji wa meli za uvuvi kwa kutumia mfumo wa kielekroniki (Electronic Monitoring System) kwa kufunga kamera kwenye meli.

vi. DSFA kwa kushirikiana na taasisi za utafiti nchini itaendelea kuwezesha tafiti katika bahari kuu ili kuimarisha uhifadhi, usimamizi, udhibiti na uendelezaji wa uvuvi kwa ajili ya kuchagiza ongezeko la mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa na kuboresha kipato kwa jamii ya wavuvi.

## PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MALIASILI ZA BAHARI

88. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza programu za utoaji elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati shirikishi za uvuvi Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari katika maeneo ya uhifadhi.

ii. Kuimarisha Doria/Ulinzi shirikishi 340 katika maeneo ya Maji ya Ndani kwa kununua boti 7 za doria (3 kubwa na 4 ndogo) ili kudhibiti Uvuvi haramu.

iii. Kukamilisha utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya mawili ya hifadhi Pemba Kaskazini Mashariki na Kusini Mashariki.

iv. Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ada za kiingilio katika maeneo ya Hifadhi.

v. Kuendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira ya baharini.

**89. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 3,700,000,000** kwa ajili Programu ndogo ya Uhifadhi. Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 700,000,000** Mishahara na **Shilingi Bilioni 3,000,000,000** ambapo **shilingi Milioni 300,000,000** Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 2,700,000,000** "Retention" ya Makusanyo ya Idara ya Uhifadhi.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**90. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi lengo lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ustawi na ufanisi wa sekta. Programu imegawika katika programu ndogo tatu nazo ni:

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti

iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba

91. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 3,664,900,000** kwa ajili ya Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 2,314,900,000** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi Bilioni 1,350,000,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi na miundombinu ya mawasiliano.

ii. Kufuatilia na kudhibiti Mali za Serikali

iii. Kusimamia utendaji kwa kuandaa na kutekeleza mpango wa rasilimali watu, mpango wa mafunzo, mpango wa manunuzi, ripoti ya fedha, ukaguzi na kazi za kamati za menejimenti za Wizara.

iv. Kutayarisha na kusimamia mkataba wa huduma kwa mtaka huduma

93. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 1,800,000,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1,000,000,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 800,000,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa agenda ya Utafiti ya Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hiyo.

ii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali katika ukusanyaji na usambazaji wa Takwimu.

iii. Kushirikiana na Tume ya Mipango katika Kuandaa na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi pamoja na kusimamia miradi ya Wizara itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

iv. Kuandaa Mpango kazi, bajeti ya Wizara na Ripoti za Utekelezaji kwa kila robo mwaka.

v. Utekelezaji wa kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vi. Kufanya Ufuatiliaji wa Programu/Miradi ya Maendeleo kwa kila robo mwaka.

vii. Kuandaa miradi mipya ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kuratibu usimamizi wa miradi inayoendelea ya wizara.

viii. Kuratibu vikao vya Mashirikiano ya Wizara kwa SMT na SMZ pamoja na mashirikiano ya ndani, kikanda na kimataifa.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Milioni 470,000,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.

Kati ya fedha hizo **Shilingi Milioni 190,000,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 280,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA

**96. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**97. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu Vikao vinne (4) na Ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Wizara Pemba.

ii. Kufanikisha Ziara za Viongozi wa Wizara Kitaifa pamoja na Sherehe za Kitaifa.

iii. Ufuatiliaji na utekelezaji wa Kazi za Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba.

iv. Kuratibu na kufanikisha Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu Pemba.

v. Kuimarisha Mashirikiano na Taasisi Nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za Kijamii.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi Bilioni 1,394,900,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba kwa Matumizi ya Kazi za Kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi **Bilioni 1,124,900,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 270,000,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi Bilioni 11,273,214,000** kupitia vianzio vyake vitano (5) vya Unguja na Pemba.

**100.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 172,033,961,377.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 14,952,100,000** kwa Kazi za Kawaida ambapo **Shilingi Bilioni**

**4,404,900,000** Mishahara, **Shilingi Bilioni 5,926,500,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi Bilioni 4,620,700,000** ni ruzuku kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar. Kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 157,081,861,377.** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 131,245,370,000** SMZ na **Shilingi Bilioni 25,836,491,377** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambapo **Shilingi Bilioni 23,138,491,377** ni mkopo na **Shilingi Bilioni 2,698,000,000** ni ruzuku.

## HITIMISHO

**101. Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa nachukua nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika utekelezaji wa programu na utoaji huduma za Uchumi wa Buluu ikiwemo sekta za Uvuvi, Ukulima wa Mwani, Ufugaji wa Mazao ya Baharini, Utafiti,Uhifadhi wa Bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais (Ikulu); Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera,

Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wamekuwa karibu sana nasi katika kulipeleka mbele gurudumu letu la maendeleo ya Uchumi wa Buluu; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ikiwemo pia wadau wetu wa karibu kabisa wa Uchumi wa Buluu ambao ni KMKM; Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ikiwemo ZIPA; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**102. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inatoa shukrani zake za dhati na za kipekee kwa wadau wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa Mipango yake ya Uchumi wa Buluu. Taasisi hizi ni pamoja na

Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano; Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT; Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT), ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania; Wizara ya Nishati SMT; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT). Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walio mstari wa mbele katika kuutangaza Uchumi wa Buluu duniani kote.

